CHILD MARRIAGE FREE WORLD

# Tamko la wanasheria/waharakati kumaliza ndoa za utotoni

Sisi ni wanasheria/wanaharakati waliopitia ndoa za utotoni kutoka Afrika na Asia ambao kibinafsi tumepitia madhara makubwa ya ndoa za utotoni. Pamoja, tunabeba sauti za maelfu ya wanawake na wasichana ambao hadithi zao mara nyingi zinanyamazishwa.

Tumeungana ili kushirikisha ujuzi wa uzoefu wetu juu ya mabadiliko yanayohitajika haraka kumaliza ndoa za utotoni na kutoa mfumo thabiti wa msaada wenye viwango vingi kwa wahasiriwa unaotambua maumivu yetu na kutupa nguvu ya kustawi. Hakuna msichana mwengine yeyote anapaswa kuendelea kuvumilia kile tulichopitia au kile bado tunaendelea kupitia. Hali ni ya dharura, na suluhisho ziko mikononi. Wakati wa kuchukua hatua ni sasa.

## Mabadiliko yanayohitajika kuzuia ndoa za utotoni ili wasichana wawe na maisha salama na mustakabali wenye nguvu zaidi:

### Toa haki ya elimu ya bure, yenye ubora, salama na inayopatikana kwa kila msichana hadi umri wa miaka 18.

- Uangalizi maalumu na uwekezaji lazima ufanyike kwa wasichana wanaoishi katika jamii za vijijini au mbali, pamoja na programu maalumu kwa wasichana waliyoacha shule awali ili kurudi masomoni.
- Elimu lazima ijumuishe mafunzo ya kitaalamu, ujuzi wa kiuchumi na wa maisha, pamoja na elimu ya afya ya uzazi na ngono inayofaa umri husika, ili wasichana waweze kufanya maamuzi sahihi na kulinda uhuru wa miili yao.
- Jitihada lazima zichukuliwe ili kupunguza pengo la kidijito ili kuwezesha upatikanaji sawa wa taarifa, mafunzo na kujieleza na pia kuwa na nafasi salama za kimwili na kidijito kwa wasichana kuungana, kujifunza na kushirikiana.

### Kuwezesha jamii kushiriki kikamilifu katika kuzuia ndoa za utotoni na kupinga mila hatari za kijinsia:

- Makundi ya kimsingi, mashirika yanayotokana na jamii, na wanaharakati wanaojua jamii zao vizuri zaidi lazima washirikishwe moja kwa moja kufanya shughuli za uhamasishaji shuleni, katika maeneo ya kidini na mikutano ya kijamii inayofikia watoto na watu wazima.
- Kampeni kubwa za uhamasishaji juu ya haki za wasichana na dhidi ya dhana potofu za kijinsia, na katika kukomesha mienendo ya kulipia mahari yenye madhara zinapaswa kufanywa kwa njia za kuvutia na zinazoweza kueleweka, kama vile kutumia muziki, tamthilia, maonyesho ya barabara au mabango na kuhusisha wadau mbalimbali kama vile viongozi wa jamii, viongozi wa kiasili na kidini, pamoja na wavulana na wanaume kama washirika.
- Wasichana wenyewe wanapaswa kushirikishwa kikamilifu katika kufanya maamuzi yanayowahusu, kupitia vilabu, mijadala, au mabaraza ya vijana, kuwawezeshq kuwa mawakala wa mabadiliko.

### Kutunga na kutekeleza sheria zinazoweka umri wa kisheria wa ndoa kuwa miaka 18 kwa wasichana na wavulana, bila ubaguzi.

- Serikali lazima ziwekeze katika mafunzo kwa maafisa wa mitaa, polisi na majaji ili kutekeleza sheria hizi kwa uthabiti na kwa heshima, pamoja na kutekeleza njia zinazopatikana, za siri, na za kirafiki kwa watoto kuripoti vitisho vya ndoa za utotoni bila hofu ya kisasi.
- Sheria dhidi ya aina nyingine za ukatili dhidi ya wasichana, kama vile unyanyasaji wa kijinsia na kingono, zinapaswa kuimarishwa na kutekelezwa.
- Uhamasishaji juu ya sheria na matokeo yake lazima uongezwe kwa wadau mbalimbali, hasa wazazi.

### Komesha umasikini wa kipekee ili kupunguza shinikizo la kifedha kwa familia zilizoathirika ambazo zinaweza kusababisha ndoa za utotoni.

- Tekeleza msaada wa kifedha unaolenga familia zilizo hatarini, kama vile michango ya fedha iliyo na masharti inayohusiana na kuhudhuria shule kwa wasichana.

## Mabadiliko na miundo ya msaada inayohitajika kwa ajili ya manusura wa ndoa za utotoni kupona na kujenga maisha yao upya:

**Manusura lazima wapewe msaada wa kikamilifu ili warudi katika jamii zao, kupata elimu na/au ajira bila ya unyanyapaa au ubaguzi.**

- Upatikanaji wa msaada wa kifedha kama vile mikopo ya elimu, ufadhili wa miradi, ruzuku za ujasiriamali na programu za kuwekwa kazini lazima upatikane kwa manusura ili waendelee na elimu yao, wapate nguvu mpya katika malengo yao na kusaidia kufikia uhuru wa kifedha.
- Shule na mahali pa kazi lazima ziweke programu za kupinga dhuluma za wanafunzi au wafanyakazi, na pia programu za kuwarudisha kwa heshima manusura ili kuepuka kutojumuishwa au unyanyapaa, na jamii zinafaa kuhakikisha ya kuwa manusura wanashughulikiwa kwa heshima!
- Programu za elimu za kuwapa manusura nafasi ya pili, mafunzo ya kiufundi na shughuli zinazotoa kipato zinapaswa kutengenezwa kwa ajili ya manusura hawa, kama vile ratiba zinazobadilika na msaada wa utunzaji wa watoto kwa akinamama wachanga.

**Waathirika lazima wapate usaidizi wa bure, unaoendelea, salama na wa siri wa afya na kisaikolojia ili kushughulikia majeraha yao ya kihisia.**

- Ushauri nasaha wa muda mrefu na huduma nyingine za afya ya akili, kama vile makundi ya msaada yanayoongozwa na marika, lazima ziwe za bure au zenye gharama iliyopunguzwa na zitolewe na wataalamu waliofunzwa juu ya kihoro (trauma) na ukatili wa kijinsia.
- Watoaji huduma wote – kuanzia madaktari na walimu hadi ofisa wa polisi na wafanyakazi wa kijamii– lazima wapewe mafunzo ya kutambua dalili za kihoro (trauma), kujibu kwa huruma, na kuepuka kuwapitisha manusura kwa kihoro (trauma) upya.
- Upatikanaji wa huduma za afya ya ngono na uzazi bila upendeleo lazima uhakikishiwe kwa manusura, ikiwa ni pamoja na utunzaji kwa wale waliopata ujauzito mapema au kujifungua mapema.

**Manusura lazima wapate msaada wa kisheria wa bure na msaada mwingine wa nyenzo ili kuwezesha upatikanaji wa haki.**

- Msaada wa kisheria lazima ujumuishe kurekebisha madhara yote ya ndoa za utotoni, ikiwa ni pamoja na kufutwa kwa ndoa, talaka na kesi za malezi ya watoto.
- Manusura na mashahidi lazima walindwe kwa usalama wakati wa taratibu zote za kisheria.

**Programu za msaada na utetezi zinazoongozwa na manusura lazima ziwe na ufadhili kamili na kuungwa mkono kitaasisi.**

- Mitandao ya msaada wa jamii inatoa uelewa muhimu, mshikamano, na nguvu za pamoja zinazotoa athari ya muda mrefu, na inapaswa kuhusisha viongozi wanawake, marika nawanasihi (mentors) waliofunzwa.
- Majukwaa ya manusura kuongoza utetezi dhidi ya ndoa za utotoni na kushirikisha uzoefu wao wa maisha lazima lianzishwe; sauti zao ni zenye nguvu na lazima zisikilizwe.

## *Imepigwa saini na:*

**Tunasihi watoa maamuzi katika ngazi zote kusikiliza mapendekezo yetu. Kila mtoto mdogo akiyefanywq kuwa mke anawakilisha si tu mtoto aliyenyang'anywa utoto wake, elimu na mustakabali wake, bali pia uwezo uliopotea kwa familia yake, nchi yake, na ulimwengu.**

**A.M**, *Zimbabwe*
**Ahumuza Martha,** *Uganda*
**Bhumi,** *India*
**Doreen Mugabiirwe,** *Uganda*
**Glodie Mikohe**, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo
**Grace Nalumbwe**, *Zambia*
**Kumah Naomi Elorm,** *Ghana*
**Mariatu Koroma,** *Sierra Leone*
**Nisha D,** *India*
**Nisha R,** *India*
**Njavwa Nakamba,** *Zambia*
**Rabina Risidev,** *Nepal*
**Rami Kumari Ram,** *Nepal*
**Rukman**, *India*
**Ruvimbo Topodzi,** *Zambia*
**Salrica Mary Conteh,** *Sierra Leone*
**Samantha Chidodo,** *Zimbabwe*
**Sugana,** *India*

CHILD MARRIAGE FREE WORLD